

REF: PPR/11 - 2/10

**TAARIFA KWA UMMA KUHUSU BEI KIKOMO ZA MAFUTA AINA YA PETROLI KUANZIA
TAREHE 24 OKTOBA 2011**

Mamlaka ya Udhhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA) inatangaza bei kikomo za bidhaa ya mafuta ya petroli hapa nchini. Bei hizi zitaanza kutumika kuanzia **Jumatatu, Tarehe 24 Oktoba 2011**. Pamoja na kutambua bei kikomo za bidhaa mbalimbali za petroli nchi nzima, ni muhimu kuzingatia yafuatayo.

- (a) Bei za jumla na rejareja kwa aina zote za mafuta zimebadilika ikilinganishwa na toleo lililopita la tarehe 10 Oktoba 2011. Katika toleo hili, bei za rejareja kwa aina zote za mafuta zimeshuka kama ifuatavyo: Petroli imeshuka kwa TZS 69.34/lita sawa na asilimia 3.36; Dizeli imeshuka kwa TZS 35.54/lita, sawa na asilimia 1.76 na Mafuta ya taa imeshuka kwa TZS 20.49/lita, sawa na asilimia 1.04. Mabadiliko haya ya bei za mafuta hapa nchini yametokana na kushuka kwa bei katika soko la dunia na kushuka kwa thamani ya Shilingi ya Tanzania ikilinganishwa na dola ya Marekani, (sarafu ambayo hutumika katika manunuzi ya bidhaa za mafuta kwenye soko la dunia). Bei za aina zote za mafuta zingeshuka zaidi kama thamani ya shilingi isingendelea kushuka ikilinganishwa na dola ya marekani ambapo, kwa kulinganisha toleo hili na toleo lililopita thamani ya shilingi katika toleo hili imepungua kwa asilimia 2.39. Bei za jumla kwa kulinganisha matoleo haya mawili zimebadilika kama ifuatavyo: Petroli imeshuka kwa TZS 69.33/lita sawa na asilimia 3.47, Dizeli imeshuka kwa TZS 35.54/lita, sawa na asilimia 1.82 na bei ya Mafuta ya Taa imeshuka kwa TZS 20.49/lita, sawa na asilimia 1.07.
- (b) Kwa mujibu wa Sheria ya Mafuta ya mwaka 2008, bei za bidhaa za mafuta ya petroli zitaendelea kupangwa na soko. EWURA itaendelea kuhamasisha ushindani kwa kutoa taarifa za bei kikomo za bidhaa za mafuta. Taarifa hizi zina lengo la kuwasaidia wadau kufanya maamuzi stahiki kuhusu manunuzi ya bidhaa za mafuta.
- (c) **Kampuni za mafuta zipo huru kuuza bidhaa za mafuta ya petroli kwa bei ya ushindani ilimradi bei hizo ziko chini ya bei kikomo (price cap)** kama ilivyokokotolewa na *fomula* iliyopitishwa na EWURA na ambayo ilichapwa kwenye Gazeti la Serikali Na. 5 la tarehe 9 Januari 2009 na marekebisho yaliyofanywa kupitia Tangazo la Serikali Na. 216 la Tarehe 29 Julai 2011.
- (d) Vituo vyote vya mafuta vinatakiwa kuchapisha bei za bidhaa za mafuta katika mabango yanayoonekana bayana na yakionyesha bei ya mafuta, punguzo, vivutio vya biashara au promosheni zinazotolewa na kituo husika. Pale ambapo inawezekana kuchagua, wateja wanashauriwa kununua bidhaa za mafuta kutoka kwenye vituo vinavyouza mafuta kwa bei ndogo zaidi ili kushamirisha ushindani. **Ni kosa kuuza mafuta bila kuweka mabango ya bei inayoonekana vizuri kwa wateja na adhabu itatolewa kwa kituo husika.**
- (e) Wanunuzi wanashauriwa kuhakikisha kuwa wanapata stakabadhi ya malipo inayoonesha jina la kituo, tarehe, aina ya mafuta yaliyonunuliwa na bei kwa lita. Stakabadhi hiyo ya malipo itatumika kama

kidhibiti cha mnunuzi wa mafuta endapo kutajitokeza malalamiko ya ama kuuziwa mafuta kwa bei ya juu kuliko bei kikomo; ama endapo utakuwa umeuziwa mafuta yenye kiwango cha ubora kisichofaa.

A: BEI ZA REJAREJA

Mji	Bei Kikomo		
	Petroli (TZS/LT)	Dizel (TZS/LT)	Mafuta ya Taa (TZS/LT)
Dar es Salaam	1,994	1,980	1,956
Arusha	2,078	2,064	2,040
Arumeru	2,078	2,064	2,040
Karatu	2,096	2,083	2,058
Monduli	2,083	2,070	2,045
Ngorongoro (Loliondo)	2,155	2,141	2,117
Kibaha	1,999	1,985	1,960
Bagamoyo	2,005	1,992	1,967
Kisarawe	2,001	1,988	1,963
Mkuranga	2,004	1,990	1,965
Rufiji	2,022	2,008	1,983
Dodoma	2,053	2,039	2,014
Kondoa	2,085	2,071	2,047
Kongwa	2,050	2,036	2,012
Mpwapwa	2,054	2,040	2,016
Iringa	2,058	2,044	2,020
Kilolo	2,062	2,049	2,024
Ludewa	2,124	2,110	2,086
Makete	2,117	2,103	2,079
Mufindi	2,068	2,054	2,029
Njombe	2,086	2,073	2,048
Bukoba	2,209	2,195	2,171
Biharamulo	2,183	2,169	2,145
Karagwe	2,225	2,211	2,187
Muleba	2,200	2,186	2,162
Ngara	2,174	2,161	2,136
Misenyi	2,217	2,203	2,179
Kigoma	2,225	2,211	2,187
Kasulu	2,211	2,197	2,173
Kibondo	2,189	2,175	2,151
Moshi	2,068	2,054	2,029
Hai	2,071	2,057	2,032
Mwanga	2,061	2,047	2,022
Rombo	2,089	2,075	2,051
Same	2,054	2,040	2,015

Siha	2,074	2,061	2,036
Lindi	2,053	2,039	2,014
Kilwa Masoko	2,028	2,014	1,989
Liwale	2,074	2,060	2,036
Nachingwea	2,082	2,068	2,044
Ruangwa	2,080	2,066	2,042
Babati	2,116	2,102	2,078
Hanang	2,127	2,113	2,089
Kiteto	2,127	2,114	2,089
Mbulu	2,129	2,115	2,091
Simanjiro	2,148	2,134	2,110
Musoma	2,172	2,159	2,134
Bunda	2,163	2,150	2,125
Serengeti	2,218	2,204	2,180
Tarime	2,183	2,170	2,145
Mbeya	2,101	2,087	2,062
Chunya	2,110	2,097	2,072
Ileje	2,114	2,100	2,076
Kyela	2,117	2,103	2,078
Mbarali	2,085	2,071	2,047
Mbozi	2,110	2,097	2,072
Rungwe	2,110	2,096	2,071
Morogoro	2,019	2,005	1,981
Mikumi	2,035	2,021	1,996
Kilombero	2,057	2,043	2,019
Mahenge	2,067	2,053	2,029
Kilosa	2,037	2,023	1,999
Mvomero	2,029	2,015	1,991
Mtwara	2,066	2,053	2,028
Masasi	2,092	2,078	2,053
Newala	2,098	2,084	2,060
Tandahimba	2,091	2,077	2,053
Mwanza	2,144	2,130	2,105
Geita	2,185	2,171	2,147
Kwimba	2,180	2,166	2,142
Magu	2,152	2,138	2,113
Misungwi	2,149	2,136	2,111
Sengerema	2,176	2,162	2,138
Ukerewe	2,203	2,189	2,165
Sumbawanga	2,167	2,153	2,129
Mpanda	2,201	2,187	2,163
Nkasi	2,180	2,166	2,142
Songea	2,117	2,104	2,079
Mbinga	2,151	2,137	2,113
Namtumbo	2,146	2,132	2,108

Tunduru	2,176	2,162	2,138
Shinyanga	2,123	2,109	2,084
Kahama	2,136	2,123	2,098
Bukombe	2,148	2,135	2,110
Bariadi	2,164	2,150	2,126
Kishapu	2,151	2,137	2,113
Maswa	2,155	2,141	2,117
Meatu	2,162	2,148	2,124
Singida	2,084	2,071	2,046
Iramba	2,097	2,083	2,058
Manyoni	2,069	2,055	2,031
Tabora	2,148	2,134	2,110
Igunga	2,102	2,088	2,063
Nzega	2,112	2,099	2,074
Sikonge	2,160	2,146	2,122
Urambo	2,161	2,147	2,123
Tanga	2,040	2,026	2,002
Handeni	2,031	2,017	1,993
Kilindi	2,054	2,040	2,016
Korogwe	2,033	2,019	1,995
Lushoto	2,043	2,029	2,005
Mkinga	2,054	2,040	2,016
Muheza	2,040	2,026	2,002
Pangani	2,047	2,033	2,008

B: BEI ZA JUMLA

Bei za Jumla - DSM	Petroli	Dizeli	Mafuta ya Taa
Bei Kikomo	1,926.48	1,912.96	1,888.04


 Eng. Mutaackulwa Mutegeki
 Kny: MKURUGENZI MTENDAJI
 EWURA